

Mtaala Endelevu wa Kitaifa (NSC)



**MKUTANO MKUU WA SABA WA WADAU WA
KAHAWA KITAIFA: MEI 2016, MOROGORO**

Utangulizi



❑ Mtaala endelevu wa Kitaifa (NSC)

- Ni kitini kilichounganishwa, chenye mwongozo wa utoaji huduma za ugani kwa ajili ya uzalishaji endelevu wa zao la kahawa

❑ Mchakato wa mtaala ulianzishwa na wadau wa kahawa nchini mapema mwaka 2015 kutokana na majadiliano/mashauriano yaliyofanyika kwenye kanda 8 za uzalishaji

- Mtaala sasa umekamilika, kinachofuata ni Uzinduzi na Usambazaji kwa ajili ya matumizi (ikiwa ni pamoja na kuweka mtandaoni)

Mtaala: Wadau waliohusika

□ Vikao vya majadiliano/mashauriano vilihusisha wajumbe wa kamati za wadau za kila kanda:

- Bodi ya Kahawa Tanzania : Mdau kiongozi
- Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania
- Wawakilishi toka serikali za mitaa
- Washauri wa Kilimo wa Mikoa
- Wakulima wawakilishi
- Makampuni
- Mashirika yasiyo ya kiserikali na
- Wadau wengine kwenye sekta binafsi



Mtaala: Mchakato wa uundwaji

- Kamati kuu ya kitaifa ya uendelezaji wa zao la Kahawa imekutana mara kadhaa kusimamia zoezi la uandaaji wa mtaala na kushauri
- Mikutano ya mara kwa mara ya kamati ndogo kumsaidia mshauri aliyeandika mtaala
- Ushiriki mahususi wa wadau wote wa kahawa katika kutoa maoni yao kwenye rasimu za awali za andiko la mtaala

Mchakato wa uundwaji ...

- Rasimu nne za mtaala ziliwasilishwa na mshauri
- Majaribio ya mtaala: Kilimanjaro na Kagera
- Uundwaji wa kamati ya 'Mtaala Endelevu wa Kitaifa' (TCB, TaCRI, LGA, Sekta binafsi) kwa usimamizi wa utekelezwaji wa mtaala
- Kamati kuu ya kitaifa ya uendelezaji wa zao la kahawa kupitia upya hadidu za rejea na mpango mkakati wa mradi endelevu wa kitaifa wa kahawa

Mtaala: Hatua zinazofuata

- Maandalizi na uzinduzi wa mtaala katika kanda za uzalishaji wa kahawa
- Majaribio ya mtaala na usambazaji kwa ajili ya matumizi kwenye kanda tatu (Mbeya/Katavi, Ruvuma na Kagera)
- Uundwaji wa kamati ndogo ya mtaala kwenye kanda chini ya kanuni za TCB itakayosimamia majaribio kwenye kanda
- Uandaaji wa hadidu za rejea kwa ajili ya kamati ndogo ya mtaala kwenye kanda za majaribio

Hatua zinazofuata

- Kufanya upembuzi wa awali na kuandaa mkakati kwa ajili ya kufanya tathmini na ufuatiliaji
- Kamati ndogo ya mtaala na kamati za kanda wanachagua wilaya za majaribio, wakufunzi na washiriki wa mafunzo
- Uandaaji wa hadidu za rejea kwa wakufunzi kwenye kila kanda ya majaribio
- Kufanya mafunzo kwenye kila wilaya teule za majaribio
- Kuendelea kushauriana na taasisi za kitaifa katika utekelezaji wa mtaala

Mtaala: Mbinu za utekelezaji

- Mafunzo yatakuwa shirikishi
- Washiriki / maafisa ugani kutoka sekta binafsi na umma (30 kutoka kila kanda)
- Mafunzo kwa vitendo kulingana na kalenda ya Kahawa
- Baada ya mwaka huu, tunashauriana na wadau kwa ajili ya kuusambaza mtaala nchi nzima

Asante sana kwa kusikiliza!

